

Usilie Mtoto Maa Kumekucha



Dalmas S. Kapurua

Maneno Mapya

Nginyira (Maasai) - Aina ya viatu vinavyotengenezwa kwa kutumia magurudumu ya gari.

Ronkena (Maasai) - Aina ya nyama iliyokaushwa kwa mafuta

Inkishu (Maasai) - Ng'ombe

Usilie Mtoto Maa Kumekucha

Dalmas S. Kapurua

**Usilie Mtoto Maa Kumekucha
Chapa ya kwanza 2015**

ISBN: 978-9966-081-67-4

Barua pepe: *senterod2011@gmail.com*

Nambari ya simu: +254 700 412 943

Haki miliki ni ya *Dalmas S. Kapurua*

Printed by **Kenyatta University Press (KUP)**

P.O Box 43844-00100 Nairobi, Kenya

UTANGULIZI

Nakala hii imeandikwa kwa lugha rahisi inayoeleweka kwa wote bila usumbufu wa kina katika utafiti wa maneno magumu, misemo, methali, mafumbo na lugha yote kwa jumla.

DIBAJI

Riwaya hii inahusu maisha ya kijana Macho. Maisha yake ilikuwa ngumu na yenye changamoto yasiyo kifani. Alizaliwa kwa shida na kukulia kwa shida. Hatimaye, baada ya kuangukiwa na kikuti kibichi, anapata kisomo kidogo. Licha ya visa vya vifo vilivyomtangulia awali kumjaribu kumchukua akiwa na mama yake, hakuvunjika moyo kwani aliona matumaini makubwa na makuu ya kubadilisha maisha yao, bila kujali udhaifu wao wa kila hali uliowaandama.

Kwa wepevu, jamii aliyotoka Macho, ilikuwa jamii inayoagaliwa kama nyonge ambayo inakosa maarifa ya lazima kwa dunia ya sasa. Na ndiposa, visa kama unyanyasaji, kunyang'anywa uongozi, kutapeliwa wauze ardhi yao pana na nzuri, kwa pesa duni. Shule zao zinazambaratishwa kwa njia zisizo na maana, na kwa yote wanafanyiwa unyama kama vile kuuliwa ovyoovyo, mabinti wao kubakwa na hakuna hatua linalochukuliwa kwa wale wanaosababisha visa hivi. Lakini mwishowe, tunaona jamii ya kina Macho inaokoka mashida haya yote, na maisha yao ikarudi raha mustarehe kutokana na ukombozi wa Macho, uliofuatia kisomo kidogo alichokipata.

Namaliza dibaji hii kwa kumshukuru Bw Dalmas Kapurua kwa kunipa heshima ya kuiandikia dibaji riwaya hii. Aidha nampa pongezi kwa juhudi na mafanikio yake, ambazo tunaawachia wasomaji na wakwasi wengine wa lugha ya Kiswahili wayaweke kwenye uzani na kuyatadhimini. Nina hakika kazi hii itawashughulisha na kuwafikirisha nyinyi wanajamii kwa miaka ijayo.

Lakini nalipa jamii jukumu hili hasa nikimulika serikali ya kaunti, wajaribu kuikuza na kuwapa moyo waandishi hawa wenye umri mdogo, waliobarikiwa na maarifa na kwa yote, kipaji cha kukitengenezea jamii kioo kizuri kama hiki, cha kujitazama ili waweze kuyadondoa madosari yanayokuwa tisho kisha kuifanya jamii izichukuwe sura nzuri na inayong'aa. Hivyo basi, vipawa hivi visaidiwe kwa kutafutiwa masomo mazuri ya hali ya juu, inayoendanisha na vipaji vyao. Hata kama sio hapa nchini, watafutiwe nafasi km. Katika chuo kikuu cha Dar es salaam (TZ), Chuo cha Ohio (Umarekani) na vingine vitakavyowapa usaidizi wowote nzuri na bila shaka, jamii na hata nchi yote kwa jumla itapata manufaa, heshima na faida chekwa kutokana na vipaji hivi. Bw. Sammy Mula Ntiapuyu (Shada ya uzamili, Chuo kikuu cha Nairobi.



Ni ukweli kilio chetu kitamfikia. Atatusikia na atatufikia. Lakini, tukizambaratisha kilicho cha asilia yetu, bila kujali kesho yetu, tutaishi vipi? Nani atatudhamini tena? Historia yetu ataheshimu nani tena? Ni mambo ya kutahadhari kabla ya athari zao. Yaliyopita si ndwele tugange yajayo. Wakati ni sasa hivi, kulinda chochote kilichobaki. La sivyو.....

Bw. Dalmas S. Kapurua ni mwanafunzi wa Falsafa, Historia na Dini katika Ualimu (Chuo kikuu cha Kenyatta). Yeye pia ni mtafiti aliyebobea katika Nyanja zote za utafiti. Kando na kuwa mwandishi wa riwaya, yeye pia hupenda na hufanya ushairi na maigizo.

ISBN 978-9966-081-67-4



9 789966 081674